JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

SHULE YA SEKONDARI MAHONGOLE, S.L.P. 526 MAKAMBAKO.

VISION: Efficiency
MISSION: Learning by doing
MOTTO: Actions

Kumb Na: MAHSS/UT/U/VOL.1/49

Ndugu……..
…….
…….

YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii. Nakupongeza sana kwa kuchaguliwa na nategemea utaitumia nafasi hii ipasavyo ili kujenga historia nzuri ya maisha yako. Ni mategemeo ya shule kuwa uwapo hapa utashirikiana vizuri na walimu, watumishi wasio walimu na wanafunzi wenzako kufanya kazi za darasani na nje ya darasa. Unatakiwa kufika shuleni tarehe 11/01/2021 ili kuanza masomo yako kikamilifu na kwa wakati. Ukichelewa utaipotezaa nafasi hii adimu.

MAHALI SHULE ILIPO NA NAMNA YA KUFIKA SHULENI

Shule ipo mkoa wa Njombe, wilaya ya Njombe, halmashauri ya mji Makambako, tarafa ya Makambako, kata ya Mahongole. Ipo mashariki mwa mji wa Makambako umbali wa kilometa 27 tu. Na usafiri wa kufika hapa ni magari, pikipiki, baiskeli na aidha wanaokaa mazingira ya karibu na shule wanaweza kuja kwa mguu.

SARE ZA SHULE

Wavulana

1. Shati mbili nyeupe kabisa tetron au polista, zenye ukosi wa kawaida, mikono mifupi pamoja na tai mbili rangi ya damu ya mzee.
2. Suruali mbili rangi ya damu ya mzee, upana wa chini uwe na inchi 18, iwe na rinda mbili kila upande na mifuko mitatu, pia iwe imepindwa kwa chini (turn up) mkanda wa kuvalia suruali uwe wa ngozi rangi nyeusi (chuma cha kwenye mkanda kisiwe na urembo na maandishi ya aina yoyote, pia usiwe utambi).
3. Viatu vyeusi jozi mbili, visiwe buti, viwe vya kamba. Viatu visivyofungwa na kamba havikubaliki / haviruhusiwi.
4. Jozi mbili za soksi nyeusi.
5. Fulana moja ya dark blue (T-shirt), huvaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa, Sweta nadhifu la kijani lenye V shingoni, track suti rangi nyeusi yenye mikanda ya rangi nyeupe mikononi na raba nyeusi.
6. Viatu vya michezo.
7. Suruali nyeusi na shati rangi ya bluu (kwa wavulana watakaopangiwa nyumba zilizopo karibu na shule).

Wasichana

1. Gauni rangi nyeupe kitambaa kizito lenye mikono mirefu, kuwe na rangi ya damu ya mzee mwisho wa mikono kwa urefu wa inchi 2, kola yenye rangi ya damu ya mzee, urefu wa gauni usivuke magoti (angalia mchoro).
2. Suruali mbili mifuko miwili ya mbele pembeni rangi ya damu ya mzee.
3. Viatu vyeusi jozi mbili, visiwe buti, viwe vya kamba. Viatu visivyofungwa na kamba havikubaliki / haviruhusiwi.
4. Jozi mbili za soksi nyeupe.
5. Fulana moja ya dark blue (T-shirt), huvaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa, Sweta nadhifu la kijani lenye V shingoni, track suti rangi ya bluu bahari (light blue) yenye mikanda ya rangi nyeupe mikononi na raba nyeupe.
6. Viatu vya michezo.
7. Mashuka mawili rangi ya pinki.
8. Gauni la kijani moja na zambarau moja kwa ajili ya kushindia (shamba dress).

   NB: Hatakiwi kuja na nguo za nyumbani, awapo nje ya darasa atavaa gauni la kijani au zambarau.

9. Godoro la futi 2.5.

VIFAA VYA CHAKULA.

1. Kontena, kikombe na kijiko.
2. Ndoo ndogo kwa ajili ya usafi bwenini (kwa wasichana tu)

VIFAA VYA TAALUMA

1. Daftari kubwa (counter books) zisizopungua 10.
2. Mathematical set (mkebe), peni za kutosha, penseli, na begi la kubebea vitabu na daftari.
3. Kamusi ya Kiingereza kwa Kiswahili (Oxford English Dictionary).

VIFAA VINGINE KWA WOTE

1. Fagio la chelewa moja.
2. Karatasi ream 1 (bunda lenye karatasi 500).

HUDUMA YA CHAKULA (WANAFUNZI WA KUTWA)

MAHITAJI YA CHAKULA

i. Debe 4 za mahindi kwa mwaka, debe 2 kwa muhula.
ii. Debe 1 ½ za maharage – selunde / soya ndefu au fupi / rozi koko / kigoma kwa mwaka.
iii. Fedha taslimu 45,000/= kwa mwaka, 22,500/= kwa muhula.

NB: Mwanafunzi wa kutwa atapata mlo wa mchana tu.

WANAFUNZI WANAOKAA BWENI (HOSTELI)

MAHITAJI YA CHAKULA

i. Mahindi debe 9 kwa mwaka, debe 4 ½ kwa muhula.
ii. Maharage debe 3 kwa mwaka – selunde / soya ndefu au fupi, rozi koko / kigoma kwa mwaka, debe 1 ½ kwa muhula.
iii. Mchele kilo 20 kwa mwaka, kilo 10 kwa muhula.
iv. Fedha taslimu 85,000/= kwa mwaka, shilingi 42,500/= kwa muhula.
v. Fedha taslimu 15,000/= kwa ajili ya walimu wa Sayansi kwa mwaka.

NB: Mwanafunzi hatapokelewa kukaa bwenini kama hajakamilisha michango ya chakula.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule ni muhimu.
(b) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation) na siku za mwisho wa wiki.
(c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(h) MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU KIPINDI CHOTE AWAPO SHULENI.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
4. Uvutaji bangi na sigara
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa / kusababisha mimba
10. Kulawiti
11. Utoro
12. Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo na kutega vipindi
13. Kiburi na ukaidi
14. Kugoma / kuchochea na kuongoza mgomo
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kumiliki / kutumia simu shuleni
17. Kuchelewa kufika shuleni baada ya shule kufungua na kutoroka kabla ya shule kufungwa.

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA, UTAPOKELEWA SHULENI BAADA YA KUTIMIZA YOTE ULIYOAGIZWA. NAKUTAKIA SAFARI NJEMA, KARIBU SANA MAHONGOLE.

.....

SALUM J. MPONZI

MKUU WA SHULE

(0624 932 817 / 0763 818 767)

PRESIDENT'S OFFICE – REGIONAL ADMINISTRATIONS AND LOCAL GOVERNMENTS
MAKAMBAKO TOWN COUNCIL
MAHONGOLE SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognized hospital in respect of all new entrants of Mahongole Secondary School

Full Name …..……
Age …...……..

1.Blood comment (red & white……
2.Urine examination ….……
3.Stool examination …….
3.Syphilis test …….
4.T. B. test …….
5.Ear test ……..
4.Spleen ……
5.Abdominal……
6.Eye test ……...
Additional information or any other physical, hereditary or infectious diseases
……
……
……

Treatment after examination
……
……
……

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education.
Signature …….....
Designation ……....
Station …….....
Official stamp ……
Date ……..…….....

N.B: Fomu hii ijazwe na mganga katika hospitali inayotambulika na serikali.